

CHAAWARUL

**Wosia wa
Baba Mpenzi**

Mtakatifu Kuriakose Elias Chaawara

Wosia wa Baba Mpenzi (1868)

Original in Malayalam:

Oru Nalla Appante Chaawarul

Author

Saint Kuriakose Elias Chavara (Chaawara)

English Translation

Saju Chackalackal CMI

Kiswahili Translation

Pius Waithanje

Publisher

Chavara Central Secretariat

Chavara Hills, Kochi

150th Year Edition

© 2019 Chavara Central Secretariat

Cover Design and Layout

Fr Ajith CMI

Printing

Timothy

Chavara Central Secretariat

Chavara Hills, Kakkanad, Post Box 3105

Kochi 682 030, Kerala, India

KUTABARUKU

Watoto wangu wapendwa, mimi ni Mwana wa kiume wa Kuriakose Chaawara wa Parokia ya Mwili na Damu ya Yesu Kristu, Chennamkary. Mungu Muweza yote kwa upendo alinileta humu duniani. Vile nimezaliwa katika familia hii na wazazi hawa, ni jambo la yakini kwamba kupitia, upendo na haki sina budi kutoa shukrani na kuwatumikia. Hata hivyo licha ya matendo machache mazuri ambayo yametendwa kwa jumla, hamna jambo lolote linalodhihirika waziwazi nililo watendea. Ndiposa nawapatia waraka huu niliouandika kwa mkono wangu mwenyewe. Makala haya hayatatokomea hata baada ya mimi kufa na kuondoka duniani. Kwa hivyo nawatunukia hii hazina ya dhamani nyie wanangu wa kanisa la Kainakari. Huu ndio wosia wangu wa mwisho kwenu, wanangu, kaka zangu, wanafamilia, na watoto wote katika hali ya kimwili na kiroho. Hii iwe ishara na hakikisho

kwamba nyie ni warithi wangu. Hisani kochokocho alizowasheheneza Maulana sio ati ni kwa vile mlistahili kutokana na maisha yenu la, zimepatikana kutokana na mapenzi na imani ya wazazi wenu. Kwa hivyo mhakikishe ya kwamba hamuipotezi hazina hii. Kumbukeni kwamba nilikuja humu duniani na nikaacha wosia huu kwa kutoa nakala nyingi ilivyowezekana kwa wengi wenu ndio muuhifadhi na kuuendeleza katika nyumba zenu. Hifadhini asili yake ndani ya sanduku kanisani. Kila Jumamosi ya kwanza ya mwezi, nyote mjumuike pamoja na kuusoma, ishara ya ukumbusho wa kifo changu. Hamna jambo lingine mnalostahili kutenda ila kunikumbuka.

Kwa kumalizia, kila mwezi baada ya kuusoma wosia huu mnaweza kusema ombi fupi kwa niaba yangu “Ewe Bwana iweke roho ya mtumishi wako kwenye makao ya wenye haki.”

UTANGULIZI

Familia nzuri ya kikristo ni mfano wa mbinguni. Sababu kuu ya kuwepo kwa familia ni kuweza kuishi pamoja, wakiunganishwa na damu na upendo, watoto wakiwaheshimu wazazi wao, wakienda mbele ya Mungu kwa unyenyekevu na kila mmoja akitumainia wakovu wa milele kulingana na hali ya maisha yake. Jambo la pekee la kuliwaza mtu anayepitia majaribu na changamoto kwenye bonde la majonzi katika dunia hii, ni kwa kuishi kwenye familia ambapo upendo, utulivu na amani hupatikana. Vivyo hivyo ni jambo la kuvunja moyo kwa mtu kuishi katika familia ambamo utulivu na amani hazipatikani na ambapo hamna mtu anayejali kuhusu Mungu na wokovu wao wa milele.

Ni jambo la kuhofisha na bahati mbaya kwa familia zisizojali kuwepo kwa utaratibu mzuri kwenye nyumba zao. Ni familia ngapi za aina hiyo zilizotajiri na sifa hata

kuheshimiwa lakini zimesambaratika?
Ni mara ngapi, matendo na misimamo
ya familia hizo zimezitumbukiza kwenye
vurugu, utendaji dhambi maangamizi
na hata kifo? Nikiombea ubayana na
utulivu wa akili utokao kwa Mungu
nimeziunda hizi sheria za tabia za familia
kwa mintarafu ya kuwasaidia kuepukana
na dhambi na maangamizi yaletwayo na
kukosa tahadhari na uangalifu. Nawasihi
nyote kwa moyo mkunjufu mfuata na
mshiriki mafunzo haya kama ushauri
kutoka kwa wahenga wenu wastahiki.

Sehemu ya Kwanza

USHAURI KWA FAMILIA

Upendo

1. “Pendaneni nyote” (Jn 13:34). Msameheane makosa na upungufu wenu. Mkifanya hivyo mtakuwa na amani hapa duniani na zawadi ya milele kule mbinguni. Ni jambo la kusikitisha sana kupata familia ambayo ina ugomvi na uhasama kati ya kaka na dada. Mungu wetu amesema wazi kuwa ufalme ambao umegawanyika wenyewe utaangamizwa (Mt 12:25). Familia inayopitia hali ya ugomvi na vita kati ya watu wa familia punde itaangamia. Kama huwezi kuwasamehe watu wa familia kwa makosa yao na upungufu wao watawezaje kukusamehe wewe iwapo utawakosea siku za usoni? Kama wanastahili kukusamehe kwa makosa utakayofanya siku za usoni si hata wewe wastahili kuwasamehe kwa makosa yao

ya leo? Iwapo utawapenda wale ambao hawajakudhuru pekee, basi unalofanya ni sawa na wanayoyatenda wafuasi wa dini zingine pamoja na watu wasiojuana na hawajawahi kuonana mbeleni. Kweli yastahili wewe kwa hiari yako uzushe masaibu na matatizo mengi kuliko yale baba yetu Adam alituachia? Ole kwa wale husababisha ugomvi katika familia.

Kuna mfano wa mwanamke mzee ambaye alichocha kuwepo kwa ugomvi mwingi katika familia yake. Shetani alimtokea na kumkabithi gunialililojaadhahabunaakamchukua akaenda naye motoni kama mshauri wake akisema kuwa huyo mwanamke aliweza kukamilisha kwa muda wa siku tatu, yale yeye shetani hakuweza kutimiza kwa miaka mitatu.

Heshima na Baraka kwa familia hutokana na kuvumiliana na kuishi bila uhasama na kukaa vyema na kila mmoja. Hata wanyama huwachukia

watu wale huwatendea maovu. Uwezo wa kupuuza kasoro za wengine na kuwasamehenijambo linaloweze kana kwa wale wenye msimamo dhabiti, busara na wanao jiheshimu. Kuna wakati mmoja, mfalme Constantine alikuwa akitembea barabarani huku amezindikizwa na askari wake wa kifalme ambapo mwanaume mmoja alikuja na kumzamba kofi. Ghafla walinzi wake wakataka wapewe ruhusa kulipiza kisasi kwa kumuua huyo mhalifu. Hata hivyo mfalme aliwajibu hivi: iwapo nitafanya kama vile maafisa wadogo wangu hufanya, kuna sifa nzuri nitakayopata? Badala ya hayo ninamsamehe na hiyo ndiyo ishara ya uwezo wangu mkuu ninao kama mfalme.

2. Kesi za kifamilia zimevunja familia nyingi. Hata pale kunastahili kuwa na kesi, washtaki wengi huja kutambua kuwa ingekuwa heri kama hawakwenda mahakamani kukesi. Hamna yeyote amewahi kupata

furaha au afueni kwa kuhusika na kesi za kifamilia.

3. Kuhusika na kushiriki sherehe za ukumbusho za kifamilia siku ya Jumapili na siku zingine za faradhi za kanisa ni tendo oву ambalo hatimaye huangamiza roho. Jumapili ni siku ya Bwana. Shughuli za kiushetani siku ya jumapili ndizo huichafua siku ya Bwana. Isitoshe, ni jambo lisilostahili na linalokatazwa na Mungu na kanisa kwa waliofiwa kukosa kuhudhuria Misa na badala yake kufanya au kushiriki kwa ibada zisiso za kanisa siku ya Jumapili na siku zingine za faradhi.
4. Jiepushe na tabia ya kukopakopa pesa isipokuwa pakiwa na haja ya dharura. Ukikopa jitahidi ulipe deni haraka iwezekanavyo. Usikopeshe pesa kwa yeyote isipokuwanikwakutoamsaada. Jamii ambayo ina utajiri mwingi sana ni ile ambayo haina deni. Kama iwapo kuna madeni yaliyoachwa na

wazazi wako harakisha kuyalipa kwa roho safi kwa vile ni hatari kubwa kuyapuza. Bala kubwa huilemaza jamii ambayo ina mzigo wa madeni ambayo hayajalipwa.

Unyenyekevu

5. Usiwe na kiburi kwa sababu ya utajiri wako. Anayetangaza utajiri wake wote hadharani hujidunisha hadhi yake. Si ajabu kwa mtu anayejidai kuwa tajiri kuishia kuwa maskini mwombaji. Mfalme Daudi kwa kuwa na kiburi kutokana na nguvu zake za ajabu, alitaka kuwe na kuhesabiwa kwa watu wake. Punde si punde balaa kubwa ikawatokea watu wake kwa njia ya mpurukuto wa ugonjwa katika ufalme wake na kuwaua watu wengi sana (2Sam 24).
6. Kuwa mwangalifu katika matumizi yako; usiwe mbadhirifu wakati unaposherehekea makumbusho na sikukuu zingine. Hii ni kwa sababu hakuna mtu ajuaye unaweza

kuendelea na mtindo huu kwa muda gani – Mwanga wa taa ndogo ambayo itawekwa kwa muda mrefu ni bora kuliko mwanga mwingi kutoka kwa biwi la nyasi kavu ambalo huwaka haraka lakini kwa muda mfupi na kisha likapoa mara moja. Wakati Democritus – mwanafalsafa mashuhuri alipoulizwa ni nani aliye bora kati ya binadamu alijibu: “ambaye hana maringo na majisifu ndiye aliye mkuu.” Msomi mmoja alimshauri mtu ambaye alikuwa amefadhaishwa na ubadhilifu wa mali yake yote kupitia tafrija na sherehe za pesa nyingi na ndoa za kifahari zilizomuacha akiwa fukara. Akamwambia: “ndugu, ingekuwa hukuwakisha taa yako mchana ungeweza kuiwasha usiku kukiwa na giza.”

Jamii na Marafiki

7. Usiwe na tabia ya kuingia nyumba za majirani ukitafula umbea. Iwapo ungetekeleza majukumu ya kwako

ipasavyo haungekuwa na wasaa wa kwenda kuchunguza habari za watu wengine.

8. Usiwe na ushirika na familia ambazo hazina mpangilio wa maisha na hazimwogopi Mungu. Sio matajiri watakao kufaa kwa mambo mazuri na faraja bali ni watu wa jamii yako walio na mipango mizuri ya maisha yao na ni wacha Mungu. Ni familia ngapi zimeishia kufadhaika na kuangamia kutokana na uhusiano usiofaa na jamii tajiri? Nchini Ufaransa kuna mtu fulani ambaye alikuwa na mtoto mmoja tu wa kiume. Akafanya kila aliloweza ili huyu mvulana aoe binti ya mwanamke tajiri. Harusi ilifanyika lakini kwa masharti kwamba huyu mvulana sharti arithi mali yote ya ukoo wao. Baada ya muda Yule kijana kwa ushirikiano na familia ya bibi yake wakaanza kumdharau baba yake kutokana na umaskini wake, na hapo akafukuzwa kutoka kwa hiyo familia ya wakwe zake. Hakuwa na

lingine ila kuanza kuomba omba na akalazimika kula mabaki ya chakula kilichotupwa kutoka kwa nyumba ya mtoto wake hasa wakati kulikuwa na sherehe za makumbusho.

9. Usiwakaribishe watu wasiostahili ndani ya nyumba yako – wakaribishe tu wale wana tabia njema na ni wacha Mungu. Kama msemu maarufu usemavyo “nionyeshe marafiki wako na nitakwambia we ni nani.”
10. Wacha kila mtu ajue kwamba nyumbani mwako si mahali pa kuzungumzia lugha chafu, isiyo ya kikristu, ya ugomvi na chutuma za kuwasuta majirani ama mtu yeyote yule. Ujue kwa yakini kwamba adhabu itakupata kwa kukubali gumzo ya kuwadhalilisha majirani na matendo maovu ya watu wengine ndani ya nyumba yako. Kuna mtu mmoja aliyekuwa na mazoea ya kuzunguka akiongea maovu kuhusu wengine. Mwisho kabisa alirukwa na akili

akawa mwehu na akawa anajiuma ulimi kila wakati na hatimaye ulimi wake ukawa na vidonda vilivyoota mabuu na majipu. Mwisho kabisa alikufa kifo cha kusikitisha kutokana na maradhi hayo.

Bidii ya kazi

11. Usiwe na tamaa kubwa ya vitu na kuzidi kujiongezea vitu vya kifahari. Badala yake jaribu koboresha ulivyo navyo tayari. Utajiri wa familia haupo katika kujilimbikizia mali kochakocho ila ni kwa thamani ya vitu walivyo navyo. Mtu mmoja mwenye bidii aliweza kuishi kwa furaha licha ya kuwa hakuwa na mali nyingi. Watu wenye wivu wakamshutumu kuwa lazima awe kuna hazina aliyoficha na wakampeleka mahakamani. Mfalme akaamrisha mali yake yote ikaguliwe na iorodheshwe mara moja. Hatimaye hakupatikana na hatia alipoifahamisha mahakama kwamba hazina yake ni shamba dogo lililogeuzwa likawa dhahabu kutokana na bidii yake na

jasho lake mwenyewe.

12. Fanya kazi kutegemea wadhifa wako maishani. Kukosakufanyakazisi dalili ya mtu anayestahili kuheshimiwa ila ni sifa kwa mtu ambaye hana familia wala aila. Uzembe ndio chanzo cha maovu yote kwa kuwa humtumbukiza mtu kwa maovu mengi na mwisho humwelekeza mtu kwa tabia na mienendo isiyofaa kama vile ulevi. Pombe ni ouvu usiokubalika katika jamii na tendo lililo ovu sana mbele ya Mungu. Kathon, mtawala wa Kiroma, aliamrisha kuwa yeyote aliyetamani kuishi Roma sharti aonyeshe mikono iliyochakarika kwa kazi ngumu ili atambuliwe na akaamuru pia wateule na wakuu kila mara watembee wakiwa na zana zao za kazi wakiwa katika matembezi barabarani.
13. Biashara inachangamoto nyingi sio tu kwa hali yako bali hata kwa utajiri wako. Iwapo hauna njia nyingine ya kujipatia riziki haujakatazwa kufanya

biashara. Hata hivyo yastahili kufanywa kwa uangalifu, ukweli na haki. Hakuna mwanabiashara mdanganyifu aliyefanikiwa kupata maendeleo mazuri maishani. Utajiri uliopatikana kwa njia ya ulaghai na udanganyifu mwisho huyeyuka kama theluji na kumalizika.

Kuna wanabiashara wawili ambao biashara zao hazikuwanufaisha licha ya wao kutumia hila na udanganyifu. Siku moja walienda kwa kitubio na wakatubu kuhusu hila na udanganyifu wao. Muungamishi akawashauri wajiepushe na hila na udanganyifu. Walipofanya kama walivyoshauriwa wakapata baraka tele kutoka kwa Mwenyezi Mungu na wakafanikiwa kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Tendo la Fadhila

14. Siku zo zote ambapo hautawafadhili wengine hazitatambuliwa katika kitabu cha uzima. Ni heri watu wakupende na wakupende kuliko

wakuogope. Pasiwe na maskini yeyote atakayetoka nyumbani kwako mkono mtupu; vivyo hivyo usisite kamwe kutoa sadaka.

Kuna mtu ambaye alitenda tendo la fadhila kila siku kwa vile aliamini kuwa Mungu Muumba aliweka kama jambo la lazima kuwatendea wema watu wengine kila siku. Siku moja wakati wa chakula cha jioni alipokumbuka hakuwa ametenda wema kuwa mtu yeyote siku hiyo alienda kutimiza jambo lilo kabla ya kula chajio.

15. Ubadhirifu na ubahili ni dhabi. Mabuu yatamega utajiri wote wa mtu bahili. Vitu vya kifahari vya mtu mbadhirifu vitatokomea kama moshi. Kuna mtu mmoja aliyetumia mali yake kwa ukarimu kukidhi mahitaji ya nyumba yake na vile vile alitoa sadaka kulingana na uwezo wake. Aliendelea kutajirika na akawa hatoi

sadaka huku akimakinika sana katika kujiongezea utajiri. Punde si punde alipata kidonda cha kutisha mguuni wake. Alitafuta dawa kwa wauguzi na madakatari wengi huku akitumia pesa nyingi kwa matibabu. Hatimaye malaika akatokea na kumwambia: “fahamu kuwa wale wote ambao hujilimbikizia utajiri kwa kukataa kutoa sadaka watakumbana na hali itakayowalazimisha kutumia mali.

16. Sio lazima uwe na marafiki wengi - heri, uchague mmoja kwa uangalifu miongoni mwa watu elfu moja. Wale ambao si wacha Mungu hata wewe hawatakupenda kwa dhati. Daudi na Jonathan walipendana wakawa kitu kimoja na kushirikiana kwa dhati mpaka mwisho wa maisha yao. Mapenzi yao hayakudidimia kutokana na mambo madogo yasiyo na maana, badala yake urafiki wao ulizidi kuimarika hata wakati wa hatari na majaribu ya aina yoyote.

Kusimama na haki

17. Usidhubutu kuweka mali ya wizi nyumbani mwako hata kama ni kwa muda mfupi. Roho Mtakatifu ameonya kwamba nyumba yoyote ambayo inawekwa vitu vya wizi itachomeka. Usiambatane na wale wanaoiba kwani hawatasita kukuibia mali yako. Isitoshe, utakuwa mshiriki katika dhambi zao.

Mtu mmoja alijipatia utajiri kutokana na wizi na mambo mengine ya ulaghai. Akiwa kitandani yu hali mahatuti aliwaita watu wa kuandika wosia, kwa kisingizio kuwa alitaka kutoa wosia wa kugawa mali yake; na akasema hivi: “moyo wangu nauachia shetani.” Watoto wake walishangazwa na matamshi haya na wakataka kujua kama baba yao ana akili timamu ama alikuwa amechanganyikiwa. Naye baba yao akawajibu: “watoto wangu wapendwa nina akili timamu – sijachanganyikiwa. Nataka waandike yale ninayoyasema. ‘Naacha roho

yangu pamoja na ya mke wangu kwa shetani kwani ni yeye alinishawishi niibe mali ya watu. Nyoyo zenu vile vile nazitoa kwa shetani kwani ni kwa sababu yenu nilipora mali ya watu.”” Alipomaliza kusema haya akakata kamba.

18. Usiwanyime au ucheleweshe malipo kwa vibarua. Ni dhambi kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Usiwadhulumu wala kuwahangaisha maskini, kwani Mungu atakuhukumu kwa ajili ya kilio chao.

Inasemekana kwamba katika mji wa Leuven kulikuwa na mtu mmoja aliyekuwa tajiri sana. Mjane mmoja maskini na wanawe wane waliishi katika shamba lake kama wapangaji. Alikuwa na mazoea ya kuwahangaisha na kuwaudhi, na siku moja yule mjane akawa hawezi kuvumilia tena na akapiga magoti akaomba: “Ewe Mungu tuepushe na dhuluma na hali hii ya kusikitisha.”

Ghafla bin vu! Yule tajiri mwenye shamba akaanguka na kufariki.

Ucha Mungu

19. Kitu ambacho ni cha thamani kwa kila familia kuwa nacho ni kumcha Mungu na kumtumikia Bwana. Familia ambayo inamcha Mungu kwa dhati watavuna matunda ya baraka hapa duniani na katika aushi yao. Lugha ya kukufuru na mazungumzo ya ufidhuli yatazima mwanga wa familia iliyokuwa nzuri na kuwa kama wingu jeusi. Iwapo itawezekana shiriki ibada ya misa kila siku. Kama hilo haliwezekani, basi shiriki misa za siku ya Jumatatu kwa ajili ya nyoyo zilizo kuzimu, siku ya Ijumaa kwa ukumbusho wa mateso na kifo cha Yesu na siku ya Jumamosi kwa kumuenzi mama wetu wa huruma. Kama watu wote kwenye familia hawawezi kuhudhuria misa pamoja, basi wawe na zamu, wahakikishe kwamba mmoja ama wawili wanahudhuria misa kila siku. Ungama

dhambi zako na upokee sakramenti ya Ekaristi takatifu angalau mara moja kwa mwezi. Iwapo hutaweza kushiriki maombi ya novena yanayo husishwa na sikukuu muhimu na sikukuu za Maria Mama Yetu, ama ibada za kila mwezi kwa heshima ya Bikira Maria na Mtakatifu Yusufu kanisani, basi sharti ufanye sala hizo nyumbani.

Kuwa mwangalifu sana uweke usafi wa kiroho katika shughuli zako zote, iwe umeketi, umesimama, ukitembea, unapolala ama ukiwa unacheza. Kukosa utu humchukiza Mungu na watu duniani. Tutakuja kuelewa siku ya kiama ikifika na tuhukumiwe juu ya nyoyo ambazo ziliangamia jahanamu kutokana na mavazi ya ufidhuli ya wavulana na wasichana wanaotembea na kukumbatiana kiholela ilhali wazazi wao hawakuwarudi kwa tabia hizo.

Kulikuwa na mvulana mmoja wa

kipekee kule Ufaransa aliyekuwa mwadilifu sana. Aliweza kujiheshimu kila wakati hata akiwa peke yake. Alijisitiri mwili wake wote hata mikono. Alishikwa na hofu kuu alipoambiwa kuwa iwapo ataenda ahera ataadhibiwa kwa kukaa uchi kila wakati. Akalia sana. Kupitia kwa mfano wa huyu mvulana tunaelewa jinsi alivyojitahidi kuwa na uadilifu maishani mwake.

Subira

20. Wakati unapokumbana na majaribu, magonjwa na shida mbali mbali weka matumaini yako kwa Mwenyezi Mungu. Nguvu za mtu hazipimiki anapoonyesha uvumilivu wakati ako na furaha au mambo ni shwari. Walii mmoja alizoea kusema: “Duniani humu, mambo yote hutendeka kulingana na matakwa yangu; kwani nami matakwa yangu ni yale tu yatolewayo na Mungu.”

Wakati wa kutembelea familia,

mtakatifu Ambrose alipofahamishwa kwamba jamii fulani haijawahi shuhudia, ugonjwa, usumbufu wala msiba wa aina yoyote ile, aliondoka pale haraka akisema, “hebu tuondoke nyumba hii upesi kwani punde si punde nyumba hii itaangukiwa na janga kuu.” Papo hapo nyumba ile ikaporomoka na kuwaua wote waliokuwa ndani. Adhabu ni ishara ya upendo wa Mungu kwetu ili tuweze kumrejelea Mungu wakati wa majaribu.

Vitabu Bora

21. Vitabu vililvyoandikwa mambo ya kisayansi na watu ambao hawaamini Mungu hueneza elimu potovu na ya kijinga. Kuwa na mkusanyiko wa vitabu vya makafiri ama nyimbo chafu katika nyumba ni sawa na kuficha moto ndani ya biwi la nyasi kavu. Wazazi wanatakiwa kuwatafutia wanao vitabu vyenye busara nyumbani mwao.

Palikuwa na maskini mwombaji ambaye hakuwa amesoma. Hata hivyo alinunua vitabu kwa pesa alizopewa kama msaada, na akatafuta watu wa kumsomea vitabu hivyo na akaweza kubadilisha maisha yake kutokana na yaliyoandikwa kwenye vitabu hivyo. Aliweza kuishi maisha mazuri na akawa mfano kwa wengi.

Siku za Faradhi

22. Si vizuri mtu aridhike na kuhudhuria misa takatifu mnamo siku za faradhi. Badala yake karibu kila siku tumia wakati kwa matendo ya fadhila na wema kama vile kusikiliza mahubiri, kusoma vitabu viteule na kushiriki matendo mema, kama kuwatembelea na kuwasaidia wagonjwa, hasa walio maskini.

23. Watu utakaoajiri nyumbani kwako wawe ni wacha Mungu. Uhakikishe kwamba idadi yao ni ile tu inayohitajika. Boma nyingi zimeathirika na ushetani unaoletwa

na walioajiriwa kufanya kazi. Waajiri sharti wafahamu kuwa wanajukumu la kuwaelekeza wafanyi kazi wao kwa maisha ya kiroho.

Ratiba ya Kila Siku

24. Hakikisha umeenda kulala mapema na kuamka asubuhi bila kuchelewa. Kila mmoja sharti afuate ratiba hiyo. Kila asubuhi saa kumi na mbili kila mtu kwa familia awe ameamka na kusali maombi ya asubuhi. Kutoka hapo wale wote ambao wana nafasi wahudhurie misa ya asubuhi. Staftahi iandaliwe saa mbili asubuhi na chakula cha mchana saa sita za mchana. Njioni baada ya sala ya Malaika wa Bwana (*Angelus*), wote waseme sala kwa familia kisha wawe na nusu saa kuwazia juu ya neno kutoka vitabu vitakatifu.

Ratiba hii ya familia isikose kufuatwa hata kama kuna wageni watakao watembelea wakati huo. Hii ni kwa sababu licha ya ukweli kuwa ni vizuri

kuwakaribisha na kuwashughulikia wageni, lazima ukumbuke kuwa inakubidi uitike wito wa Mwenyezi Mungu; usisahaukamwekuwa Mungu anatazama uamuzi wako wakati kama huu. Kwa hivyo hakikisha maombi ya familia hayavurugwi au kuzuiwa na jambo lolote lile; unapofanya hivyo unakuwa mfano mwema kwa wengine, iwapo watakudhihaki kwa tabia hii jua unabaraka tele. Baada ya chakula cha jioni hapo saa mbili usiku, kuwa na muda wa kutafakari yaliyo kwa nafsi yako na useme sala ya jioni kisha uende ukalale.

Kiongozi wa familia ahakikishe kwamba maagizo haya yanazingatiwa kwa makini. Wasomee watu wa familia kanuni hizi kila jumapili na siku ya kwanza ya kila mwezi.

Sehemu ya Pili

MALEZI YA WATOTO

1. Wazazi sharti wafahamu kuwa, kulea watoto ndilo jambo lililo muhimu sana na la kimsingi katika maisha yenu. Watoto ni hazina takatifu uliyokabidhiwa na Mwenyezi Mungu. Kumbuka pia hizi ndizo nyoyo ambazo Yesu Kristu amekukabidhi mikononi mwako ili unadhifishe kwa damu yake na ili wawe watumishi wake na hatimaye waweze kumrudia siku ya kيامa. Iwapo mtoto yeyote angepotea na kwenda motoni kutokana na makosa ya wazazi wao itakuwa ni pingamizi iliyoaje kwa wokovu wao.

Origen, msomi maarufu wa dini alisema kuwa iwapo wazazi watatupwa ahera siku ya kيامa kwa sababu ya matendo maovu ya watoto wao, ni kwa sababu Mungu anawahukumu kwa matendo ya watoto wao. Iwapo unataka wanao

wawe pamoja nawe na wawe msaada wakati wa uzee wako hakikisha kwamba wamepata mafunzo mazuri ya kikristo wakiwa wachanga. Ikiwa hawatamwogopa na kumcha Mungu wakiwa wachanga, hawatawahi kuwapenda au kuwaheshimu wazazi wao. Wazazi wawakabidhi watoto wao kwa Mungu kila wakati na kuwaweka chini ya himaya ya familia takatifu na kuwaombea kila mara. Mungu atakubali maombi ya mama mzazi kama vile angekubali maombi ya mwanawe.

2. Watoto wanapokua, wafundishwe umuhimu wa kutaja kwa dhati majina ya Yesu, Maria na Yusufu. Watoto wawe na uzoevu wa kubusu, sanamu au picha za familia takatifu na wafundishwe kuheshimu na kutunza sanamu hizo.

Wanapoanza kuzungumza wafundishwe kusema sala fupi fupi kama sala ya Baba Yetu, Salamu

Maria, Malaika wa Bwana, n.k.
Ni jambo la kutia moyo sana kwa watoto kulewa na kuimarishwa kiroho kwa njia ya maombi kama vile wanavyohitaji chakula kizuri cha kujenga miili yao.

3. Usiwaache watoto wako watembe wakiwa uchi hata kama wako ndani ya nyumba. Usihusike na mazungumzo yasiyo ya heshima ama umbeya mbele ya wanao. Usione kama hawaelewi na yale unayoyasema. Watoto katika mazingira ya kikristu hata hawaambiwi kwamba walizaliwa na mama zao, wakiwa wachanga huambiwa kwamba waliletwa na mvua kutoka mbinguni ama wakaambiwa mtoto alitolewa kisimani.
4. Kwa sababu ya kuhifadhi heshima kwa watu wakubwa, watoto wasilale pamoja na wazazi wao chumba kimoja. Vile vile wavulana na wasichana wasilale chumba kimoja;

kwani mwovu shetani atawafundisha yale wasioyajua kutokana na maumbile.

5. Watoto wakiwa wachanga sana wasiruhusiwe kuwa mbali na macho ya wazazi wao wanapocheza na wenzao. Usiwaamini wafanyi kazi wa nyumbani ambao si waangalifu wakiwa na watoto na aghalabu huwaharibu.
6. Watoto wakitimiza umri ufaao, wapelekweshule. Wazazi wahakikishe kwamba wanahoji kuhusu masomo na maendeleo ya watoto wao, na vile vile wajue wanashirikiana na marafiki wa aina gani. Kila jumapili wazazi wakague yale ambayo watoto wao wamesoma.
7. Usiwaruhusu watoto wako kukaa sana kwa watu wa jamii yenu kwani inawezekana wakienda huko wawe malaika lakini wakirudi wawe mashetani.

8. Watoto wakifikisha miaka saba, hakikisha wamejua kuungama dhambi na wanashiriki shughuli hiyo baada ya kushauriwa umuhimu wake. Washauri kuhusu umuhimu wa kuheshimu na kuenzi Mama Mtakatifu.
9. Ni makosa na dhambi iwapo wazazi watakuwa wakali sana au pia kuwaachilia watoto wao. Mapenzi mengi kwa watoto yatawafanya wafurahi na wajionee fahari, hasira kuu na adhabu huishia kuwafanya watoto wakose, imani, wajidharau, na wajione wajinga.

Kabla ya kuwaadhibu watoto, hakikisha kwamba wameelezwa makosa waliyofanya na kwa nini waadhibiwe, washauriwe vilivyo huku wakipunguziwa chakula na inapostahili wapige magoti. Kuwakaripia kwa ukali na matusi hakutawasaidia watoto na badala yake kutawafanya wafuate mtindo

huo kwa watoto wao watakapokuwa wazazi. Mama apaswa kuwa kielelezo kwa watoto wake kwa kumheshimu na kumuenzi bwana yake na baba vile vile awafundhishe wanawe kwa kutoa mfano mwema wa kumpenda na kumheshimu mama yao. Iwapo baba na mama hawapendani, watoto wao hawatawaheshimu.

10. Usiwafundishe watoto kuwa wadanganyifu na kuwa na hila zingine ukidai kuwa wanahitaji kuwa wajanja ilikuishi humu duniani. Wanapokosea, warudi na uwarekebishe. Wafundishe kudhamini ukweli na haki kwa dhati.
11. Hakikisha kwamba watoto wote wamerudi nyumbani wakati kengele ya maombi ya jioni inapopigwa. Wafundishe kubusu mikono ya wakuu wao na wazazi baada ya sala za jioni. Wanapotimu miaka kumi na miwili kipindi ambacho kinahitaji tahadhari nyingi maishani mwao badala ya kuwaacha waende kwa sherehe mbali

mbalizamakumbusho, sikukuu, harusi n.k. kuwe na uangalifu na kuhakikisha kwamba wanapata mafunzo wakiwa nyumbani kushiriki majukumu mbali mbali yanayolingana na umri wao. Mambo ya wasichana kuvalia mavazi spesheli wakati wa sherehe mbali mbali au kuwa wasimamizi kwenye harusi ni desturi ambayo asili yake si ya umungu.

12. Kuwapamba mabinti zako kwa mavazi ghali na vitu vilivyopita umri na uwezo wao kama wafanyavyo matajiri na familia za kifalme huwasababishia adhabu ya moto wa jahanamu kwa viumbe hawa. Urembo wa kutamanika kwa msichana upo katika upole wake, utakatifu, ukimya na jinsi anavyoyadhibiti macho yake.
13. Watoto wanapopigana si lazima watu wazima wagombane kuhusu jambo hilo. Watu wale ambao hawawezi kustahimili wakati watoto wao wanapodharauliwa au kuumizwa na

watu wengine hudhihirisha kwamba hata wao wana hisia za kitoto.

14. Wanapokomaa kiumri, watoto wanastahili kupewa uhuru wa kujiamulia maisha wayapendayo. Hii ni kwa sababu Mungu ndiye huwa anawaongoza na ni jukumu la watoto wenyewe kufanya uamuzi unaofaa wala si jukumu la wazazi wao. Wazazi na watoto wengi wanalia wakiwa jahanamu kutokana na makosa yao kuhusu mambo hayo. Uamuzi kuhusu maisha ya wavulana yasicheleweshwe kuzidi miaka kumi na sita au kumi na nane na kwa wasichana kupita miaka kumi na nne au kumi na sita. Lazima waulizwe idhini kabla mipango ya ndoa zao haijapangwa. Katika ushirika wowote tabia njema na za kimaadili ziwe ndio mwongozo badala ya kuangalia utajiri na hadhi ya watu katika jamii. Kinyume na haya badala ya raha na buraha, matokeo yanaweza kuwa majonzi kwa watoto na wazazi wao vile vile.

15. Wazazi hawatapuuzwa wadhifa wao kwa watoto wao hata wakishakuwa wakubwa na wanajisimamia kwa mambo kadhaa. Kwa vyo vyote vile usiwaachie majukumu ya kusimamia shughuli za familia. Wazazi wengi wameishia kuhuzunika baada ya kuwaachia wanao usimamizi wa nyumba zao.
16. Kabla ya kuondoka duniani wazazi wahakikishe wamewasaidia watoto wao kuwa na makao yao wenyewe. Mali ya familia igawe kama wazazi bado wana akili zao razini. Hii ni kwa sababu ugomvi na uhasama unaweza kuibuka miongoni mwa watoto kutokana na ugomvi wa mali ya wazazi wao na wazazi hao ndio watakuwa wa kulaumiwa kwa dhambi zinazotokana na ugomvi huo.

Tamati nanyi watoto mna wajibu kutokana na amri za Mungu kuwaheshimu wazazi wenu na kuhakikisha kuwa akili zao

hazihangaishwi na mambo mabaya mnayoyafanya. Mkumbuke kwamba kuvunja amri ya nne ya Mungu kutawaletea laana kutoka kwa Mungu hapa duniani na ahera.

Nchini Ujapani katika ufalme wa makafiri paliishi mwanamke na wanawe watatu. Watoto hawa walishindwa kumtunza mama yao ilivyostahili kwa kuwa walikuwa maskini sana. Katika ufalme huu kulikuwa na sheria kuwa wezi sharti wanyongwe na wale ambao wangeshika wezi na kuwapeleka kwa utawala wa nchi wangezawadiwa vilivyo. Kwa kuvutiwa na sheria hii katika azma ya kuboresha maisha ya mama yao mtoto mmoja akajifanya mwizi nao wale wengine wawili wakampeleka kwa watawala na bila shaka wakapewa zawadi. Wakati askari jela mmoja alipoona vile wale ndugu wawili walivyomuaga ndugu yao na kumpa moyo kwamba awe na ujasiri na uvumilivu akisubiri

kifo kwa manufaa ya mama yao mzazi, akamuuliza yule aliyekuwa amefungwa ni kwa nini wale wawili wanamwonea huruma ilhali ni wao walimshtaki. Ndipo akafahamu kuwa aliyekuwa anyongweni ndugu ya wale wawili ambaye aliamua kwa hiari yake mwenyewe kufa ili mama yake aweze kuishi maisha mazuri. Wakati mfalme alifahamishwa kuhusu jambo hili, aliamuru huyo kijana aachiliwe na pia akatoa amri kuwa yule mama apewe usaidizi maisha yake yote. Wanangu wapendwa, kumbukeni kisa hiki kila wakati.

Padri Kuriakose Elias wa Familia Takatifu,
Mkuu wa Mannanam
na Monastari zingine za TOCD
Februari 13, 1868.

HISTORIA FUPI YA MTAKATIFU KURIAKOSE ELIAS CHAAWARA

Mtakatifu Kuriakose Elias Chaawara alizaliwa mnamo tarehe 10 Februari mwaka wa 1805 kule Kainakary ambacho ni kijiji kidogo cha wilaya ya Alleppey katika jimbo la Travancore. Baada ya masomo ya msingi alijiunga na seminari ya Pallipuram ya Kanisa la Mtakatifu Maria, kwa jina Cherthala. Padri Thomas Palackal ambaye alikuwa profesa wa sayansi ya dini ndiye alikuwa msimamizi wake. Alihitimu kuwa kaimu shemasi mnamo 1827 na kuwa shemasi kamili 1828. Tarehe 29 November 1829, alitawazwa kuwa padre katika kanisa la mtakatifu Andrea kule Arthunkal. Tangu akiwa mtoto mchanga Kuriakose alifundishwa kulitaja jina 'Yesu' tena na tena jambo lililomfanya atamani kujitolea maisha yake kwa Yesu na kanisa.

Baada ya kutawazwa kuwa Padri, aliungana na Padri Thomas Palackal

na Padri Thomas Porukara walio kuwa walimu wake na kuweka wakfu wa vuguvugu la kiroho la Mannanam. Baadaye Bruda Jacob Kianthara aliyependa sana walivyofurahia maisha yao ya kipekee, ya kujitenga na shughuli zote za kidunia, alijiunga nao. Walitengeneza makao yao Mannanam hapo 1831 na wakayapatia jina 'Beth Rauma' ikimaanisha, nyumba iliyoko juu ya kilima. Beth Rauma ilianza kama makao duni lakini hatimaye pakakua na kuwa makao ya kundi la mapadri waumini ambao baadaye walijulikana kama watumishi wa ujio wa imakulata. Jamii hii ya kidini pale Mannanam ndiyo iliweka msingi wa shirika la Carmelites of Mary Immaculate (CMI). Padri Thomas Palackal alikufa 1841 naye Padri Porukara akafa 1846.

Kutokana na kifo cha walimu hao wa kidini, Padri Kuriakose alipewa wadhifa wa kusimamia shirika hili jipya na akawa mkuu wake hadi kifo chake. Mnamo mwaka wa 1861, Askofu Mkuu

Bernadine wa jimbo kuu la Verapoly alimteua Padri Kuriakose kuwa Kasisi Mkuu wa wakatoliki wa Kanisa la Syro-Malabar ambapo aliweza kupambana na upinzani uliochangiwa na kufika kwa Askofu Roccas ambao ulivuruga umoja katika kanisa la Malabar.

Kuanzia mwaka wa 1831 Padri Kuriakose alijihusisha na shughuli nyingi za kiroho na za kijamii kama vile kuanzisha shule ya Sanskrit pale Mannanam iliyohusika na kuleta maendeleo ya Elimu katika eneo lile, akaanzisha mtambo wa mbao wa kwanza wa uchapishaji pale Kerala, akaimarisha utaratibu wa misa, ambapo alifanya mahubiri ya jumapili yawe ya kuvutia na kupendwa na wengi, aliandaa katika parokia mafungo ya kila mwaka kwa minajili ya watu kuimarisha ukristo wao. Mnamo mwaka wa 1866 alianzisha shirika la kwanza la kidini kwa wanawake lililojulikana kama Congregation of Mother of Carmel (CMC).

Mtakatifu Kuriakose aliishi miaka

saba ya mwisho ya maisha yake kule Koonammavu, Kerala, ambapo alikufa tarehe 3 Januari mwaka wa 1871 na akazikwa katika kanisa la Mtakatifu Philomena huko Koonammavu. Baadaye mnamo tarehe 24, Mei mwaka wa 1889, mabaki ya mwili wake yaliamishwa kutoka Koonammavu na kuzikwa tena katika kanisa ndogo ndani ya Monasteri ya Mtakatifu Yosefu kule Mannanam, makao makuu ya shirika la CMI.

Mtakatifu Kuriakose Elias alijuliakana sana kwa maisha yake ya kujinyima na bado ni mfano mwema wa kipaji cha ukristo na pia ni mfariji wa wengi wanapokumbana na majaribu na madhila mbali mbali.

Neema nyingi zimeshuhudiwa kutokana na maombezi yake. Mtakatifu Alfonsa, ambaye ni Mtakatifu wa kwana kutoka India, aliomba msaada wa maombezi ya Mtakatifu Kuriakose na papo hapo akapona ugonjwa wake. Alidhibitisha uponyo huu kwa ushuhuda aliouandika

kwa hati yake mwenyewe.

Safari ya kutawazwa kwa Padri Kuriakose Elias Chaawara ilianza hapo mwaka wa 1956 na mnamo tarehe 8, Februari mwaka wa 1986 aliteuliwa kwa matayarisho ya kuwa mtakatifu na Baba Mtakatifu John Paulo wa Pili akiwa Kottayam, Kerala.

Uponyanji wa kimiujiza wa miguu iliyopooza ya Joseph Pennaparampil kutoka Calicut, Kerala kupitia uombezi wa Mtakatifu Kuriakose kulidhihirishwa kama ishara tosha ya kutawazwa; uponyaji wa kimiujiza wa makengeza ya Maria Jose kottarathil kutoka Pala, Kerala, kuliidhihirishwa na shirika la shughuli za watakatifu la Vatican kufungua njia ya kutawazwa Mtakatifu Kuriakose. Mnamo tarehe 18 Machi mwaka wa 2014 Baba Mtakatifu Francis aliweka sahihi stakabadhi kuidhinisha mbarikiwa Kuriakose Elias Chaawara kutawazwa kuwa Mtakatifu.

Mnamo tarehe 23, Novemba mwaka wa 2014 Kuriakose Elias Chaawara alifanywa

Mtakatifu katika sherehe iliyoongozwa na Baba Mtakatifu Francis kule Roma. Kaburi ambamo mabaki ya Mtakatifu Kuriakose yamewekwa, limo chini ya altare kuu katika kanisa la Monasteri ya Mtakatifu Yusufu kule Mannanam.

SALA YA FAMILIA KWA MTAKATIFU CHAAWARA

Ewe Mungu tunakushukuru kwa kutupatia Mtakatifu Kuriakose kama mlinzi wa Familia. Sifa zote ziwe kwa Baba, kwa Mwana na Roho Mtakatifu.

Mtakatifu Kuriakose muumini mteule wa Familia Takatifu, utuombee, ili amani, upendo, umoja na ufanisi ziweze kuhifadhika katika familia zetu. Tusaidie tuweze kuimarika katika imani ya kweli na tuweze kujitolea na kunyenyekea mbele ya Mungu. Tupe nguvu ili tuweze kukabiliana na shida za maisha na moyo wa kuwa na shukurani kwa Mungu katika hali zote. Tufundishe kutegemea kudura ya Mungu pekee na kumtegemea kwa mapenzi na fadhila zake. Tujaze na ari ya kuuona ufalme wa Mungu na utupe mapenzi ya kuishi maisha yetu kwa utukufu wa Mungu. Twaomba kuongezeka kwa wito wa ukasisi na maisha ya waliotawazwa kutoka kwa familia zetu. Tunaimani na maombezi

yako ya kila mara na yenye nguvu na tunakuomba utujalie ombi hili (kwa kimya sema ombi lako) kutoka kwa Baba kwa njia ya Kristu Mungu wetu. Amina.

*(I Baba Yetu ...;
I Salamu Maria;
I Atukuzwe Baba)*

**MATUKIO MUHIMU KATIKA
MAISHA YA MTAKATIFU
KURIAKOSE ELIAS
CHAAWARA**

- 10-02-1805 Kuzaliwa Kainakary, Kerala
- 18-02-1805 Kubatizwa katika kanisa ya Parokia ya Chennamkary
- 08-09-1805 Akawekwa wakfu kama mtumishi wa mbarikiwa Bikira Maria katika kanisa la Vechoor
- 1810 Akaanza masomo ya msingi kule Kainakary
- 1818 Akajiunga na Seminari ya parokia pale Pallipuram
- 29-11-1829 Akatawazwa Padri katika kanisa la Arthunkal
- 11-05-1831 Kuanzishwa kwa shirika la kwanza la kiasili la kihindi kwa wanaume kwa jina Carmelites of Mary Immaculate (CMI) wakiwa

- pamoja na Padri Thomas Palackal na Padri Thomas Porukara
- 1831 Alifanya mahubiri ya Jumapili kupendwa na watu na kuanzisha mafungo ya sala kwa makasisi na waumini katika kanisa la Kerala
- 1833 Kuanzishwa kwa seminari ya kwanza ya jumla kwa jina Syro-Malabar kule Mannanam
- 1838 Kuanzishwa kwa njia ya msalaba kama maombi kule Mannanam
- 16-02-1844 Akateuliwa kuwa mkufunzi wa masomo ya kidini ama *Malpan* na mtahini wa maswala ya kielimu akiwa na idhini ya kutoa vibali kwa makasisi waliotawazwa ili waweze kusikiliza kitubio na kuhubiri kanisani

- 03-07-1846 Kuanzilishwa kwa mtambo wa kwanza wa uchapishaji na uandishi katika nyumba ya kanisa la Syro-Malabar kule Mannanam
- 1853 Kuanzilishwa kwa makatekisti wa kwanza wa Syro-Malabar kule Mannanam
- 08-12-1855 Kasisi wa kwanza kufunga nadhili katika kanisa kule India (akiwa na wengine 10)
- 1856-1857 Akaandika makala kumi ama Tamthilia kuhusu uchungaji akilenga kuzaliwa kwa Yesu Kristo
- 27-07-1861 Kuhusishwa na OCD kama shirika la nafasi ya tatu la Carmelites (TOCD)
- 08-06-1861 Akateuliwa kuwa kasisi mkuu katika kanisa la Syro-Malabar baada ya kipindi cha mashemasi wakuu

- 1861 Akapigania kanisa la Syro-Malabar dhidi ya mpinzani mchokozi Askofu Roccas
- 1861 Akaandika shairi simulizi la kwanza la Malayalam kwa jina *Anasthasiayude Rakthasakshyam* (*Martyrdom of Anasthasia*) ambayo ni hadithi ya kuisimua kuhusu waliouawa kwa sababu ya imani
- 1862-1869 Aliunda afisi teule kwa makasisi, akakusanya na kutunga taratibu za misa, kalenda ya ibada, afisi ya wafu, afisi ndogo ya Mama Mtakatifu n.k. katika kanisa la Syro-Malabar
- 1864 Akaanzisha ibada ya mbarikiwa Maria Bikira mwezi wa Mei kule Mannanam
- 1864 Akafanikisha mpangilio

wa ‘shule kwa kila kanisa’
katika Kanisa la Syro-
Malabar akiwa Kasisi Mkuu
 (“Kila kanisa sharti lianzishe
shule”)

13-02-1866 Wakfu wa muungano wa
waumini wanawake wa
kihindi, Muungano wa Mama
Carmel (Congregation of
Mother Carmel - CMC) kule
Koonammavu wakiwa na
Padri Leopold OCD ambaye
alikuwa Mishonari kutoka
Italia

15-02-1866 Akaanzisha ibadaya heshima
kwa Eukaristia ya masaa 40
Kerala pale Koonammavu

02-01-1868 Akaanzisha shule ya kwanza
ya malazi kwa wasichana
Kerala pale Koonammavu
wakiwa na Padri Leopold
OCD

13-02-1868 Aliandika mwongozo wa
kwanza kwa jina ‘Wosia

- wa Baba Mpenzi' (*Oru Nalla Appante Chaawarul*) uliokuwa wa kwanza na wakipekee kwa familia za wakristu katika kanisa
- 1869 Wakfu wa shirika la kwanza la waumini kwa jina 'Confraternity of St Joseph for Happy Death' kule Kainakary
- 1869 Wakfu wa makao ya kwanza ya kuwasidia wagonjwa, wazee na mayatima kwa jina Upavisala kule Kainakary
- 1869 Akaanzisha vuguvugu la muungano wa wakatoliki
- 04-05-1871 Akafariki akiwa usingizini akiwa katika monasteri ya Mtakatifu Philomena kule Koonammavu
- 04-05-1889 Mabaki yake yalifukuliwa na kuzikwa tena katika monasteri ya Mtakatifu

Yusufu kule Mannanam ambayo ndiyo ilikuwa nyumba kuu ya shirika la CMI

21-12-1936 Utaratibu wa kutawazwa kuwa Mtakatifu ukaanza katika kiwango cha shirika

09-12-1955 Utaratibu wa kutawazwa Mtakatifu ukapata idhini rasmi

03-01-1958 Mipango ikaanzishwa katika jimbo huku akipewa jina Mtumishi wa Mungu

07-04-1984 Akatajwa kama mustahiki na Baba Mtakatifu John Paul wa Pili kule Roma

08-02-1986 Hatua ya kwanza ya kutawazwa kuwa Mtakatifu (Beatification) ikaandaliwa kule Kottayam, Kerala na Baba Mtakatifu John Paulo wa Pili

20-12-1987 Serikali ya India ikatoa

stampu za posta kama ishara
ya kutambua kazi ya umma
ambayo Mtakatifu Chaawara
alifanya kwa kujitolea

04-05-2006 Picha ya Mtakatifu Chaawara
ikawekwa katika ukumbi
wa akademia ya wasomi
kule Thrissur na Serikali
ya Kerala kwa kutambua
mchango wake wa uandishi
kwa lugha ya Malayalam

14-10-2014 Kuchapishwa kwa
'Eclogues' na akademia ya
uandishi wa Kerala

23-11-2014 Kutawazwa kuwa Mtakatifu
kwa Mtakatifu Kuriakose
Elias Chaawara na Baba
Mtakatifu Francis kule
Vatican